



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

HUDUMA YA USAFIRI WAKATI WA MAONESHU YA 48 YA BIASHARA YA KIMATAIFA YA DAR ES SALAAM (48TH DITF) YATAKAYOFANYIKA TAREHE 28 JUNI – 13 JULAI, 2024 KATIKA UWANJA WA MWALIMU J.K. NYERERE, BARABARA YA KILWA – DAR ES SALAAM.

Dar es Salaam,

24 Juni, 2024.

Kutokana na kuwepo kwa mahitaji makubwa ya huduma ya usafiri kwa abiria na wafanyabiashara wanaotaka kwenda kushiriki Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa ruhusa kwa daladala kutoa huduma ya usafiri kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji kuelekea katika viwanja hivyo kwa masharti yafuatayo:

1. Daladala husika ni lazima isajiliwe LATRA na iwe na leseni hai ya usafirishaji
2. Utozaji nauli usizidi viwango vya nauli elekezi vilivyo dhinishwa na Mamlaka (LATRA)
3. Safari iwe **inaanzia** na **kuishia** katika njia ambayo daladala imesajiliwa na sio vinginevyo. Mfano, gari la Tegeta Nyuki kwenda Makumbusho kupitia barabara ya Bagamoyo litabeba abiria kutoka Tegeta Nyuki hadi Makumbusho na litaendelea na safari hadi Viwanja vya Sabasaba na kurudi tena hadi Makumbusho ili kubeba abiria waliopo Makumbusho wanaoelekea Tegeta Nyuki
4. Dereva ahakikishe anafuata Sheria zote za Usalama Barabarani kama vile, kutopakia katika eneo ambalo hakuna kituo na kufuata maelekezo atakayopewa mara afikapo viwanjani ili kupunguza foleni barabarani
5. Dereva na Kondakta wavae sare safi na nadhifu na watumie lugha nzuri kwa abiria.

MAONESHU YATAANZA TAREHE 28 JUNI – 13 JULAI, 2024.

Mamlaka inawaagiza kuzingatia mwongozo huu.

Imetolewa na:

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano